

Ndoa za wake wengi ni za ibilisi!..ndoa za wake wengi ni za ibilisi!!... ndoa za wake wengi ni za ibilisi!!!. Hali kadhalika ndoa za waume wengi ni za ibilisi, kama tu zilivyo za jinsia moja (*zote ni zao la ibilisi*).

Zipo hoja kuwa kwasababu Daudi, Sulemani na manabii wengine wakale walioa wake wengi, basi hata leo ni halali kuoia wake wengi.. tena zipo hoja zifananishazo wanyama wa porini na wa kufugwa na uhalali wa kuoia wake wengi.

Hoja zote hizi ni za ibilisi... Ndugu, usiongeze wake, wala usiongezee waume.

Bwana YESU alipokutana na yule mwanamke Msamaria kisimani hakumwambia akawaite WAUME ZAKE!.. Ingawa alikuwa ana wanaume wengi (*na Bwana alilijua hilo*), lakini alimwambia nenda “kamlete mumeo”... ikimaanisha kuwa ndoa halali na takatifu ni ya mume mmoja na mke mmoja.

Sasa Kristo alikuwa anamjua Sulemani, na Daudi..

*Yohana 4:15 “Yule mwanamke akamwambia, Bwana, unipe*

*maji hayo, nisione kiu, wala nisije hapa kuteka.*

*16 Yesu akamwambia, NENDA KAMWITE MUMEO, uje naye hapa.*

*17 Yule mwanamke akajibu, akasema, Sina mume. Yesu akamwambia, Umesema vema, Sina mume;*

*18 kwa maana umekuwa na waume watano, naye uliye naye sasa siye mume wako; hapo umesema kweli”.*

Bwana YESU kabla ya kukutana na huyu mama, alikuwa anamjua Daudi pamoja na Sulemani na idadi ya wake waliooa!.. Lakini tunaona hakumwambia huyu mwanamke Msamaria, kwamba akawaite waume zake!!.. Bali alimwambia kamlete mumeo! (*maana yake mmoja tu*).. bado huoni tu, kuwa ndoa za mitara ni batili na za ibilisi!.

Na tena biblia inasema hapo Mwanzo Mungu alimwamba mwanaume na mwanamke, na si mwanaume na wanawake, au mwanamke na wanaume (*soma Mwanzo 1:27 na Mathayo 19:4*).

Huoni kuwa ndoa hizo za wake wengi zitakukosesha maji ya uzima!.. Na pia fahamu kuwa ndoa za wake wengi sio zile tu zinazohusisha mtu kuwa na wake wengi katika boma moja kwa wakati mmoja...la! Hata zile za kuacha na kuoia mwingine ilihali yule wa kwanza bado yupo hai.. hiyo ni mitara! Ndicho kilichokuwa kwa huyu mwanamke Msamaria.

Huyu mwanamke msamaria alikuwa na wanaume watano kulingana na darubini ya kimbingu! Ingawa haishi nao, lakini alikuwa nao watano, na anayeishi naye ni wa 6, vile vile kuna watu leo hii wameacha wake zao na kuoia wengine, na kuacha tena na kuoia wengine, *(hawa hawana tofauti na wale waliooa wake wawili na kuishi nao wote kwa pamoja).*

Na madhara ya ndoa za mitara ni “KUKOSA MAJI YA UZIMA”..

Yapo maji ya Uzima tuyanywayo hapa Duniani, na yapo yale tutakayoyanywa katika mbingu mpya na nchi mpya.

Maji ya Uzima duniani ni YESU KRISTO, tumpatapo yeye tunapata uzima wa milele *(Yohana 4:14)*, lakini ukijiunganisha na hizi ndoa za mitara hawezi kuingia ndani yako!.. vile vile maji ya uzima baada ya maisha haya tutayanywa kutoka katika ule mto wa maji

ya Uzima katika mbingu mpya na nchi mpya.

*Ufunuo 22:1 “Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung’aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo,*

*2 katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa.*

*3 Wala hapatakuwa na laana yo yote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia;*

*4 nao watamwona uso wake, na jina lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao.*

*5 Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele”.*

Neema ya Bwana YESU itufunike.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

MAFUNDISHO YA NDOA.

MISTARI YA BIBLIA KUHUSU NDOA.

NDOA TAKATIFU NI MKE MMOJA/MUME MMOJA.

VIGEZO VYA KUWA KARIBU NA YESU KRISTO KATIKA ULIMWENGU  
UJAO.

NDOA NI NINI?

KUWA NA MAFUTA YOTE YA ROHO MTAKATIFU NDANI YAKO.

Rudi Nyumbani

Share on:  
WhatsApp